

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA
SHULE YA SEKONDARI MBEKENYERA**

SIMU

0783500203/0686618393

mbekenyerasecondaryschool@gmail.com



Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Mbekenyera
S.L.P. 9,
RUANGWA

Kumb Na. HWR/MBSS/E.10/VOL.II/.....

Tarehe

Jina la Mwanafunzi.....

Shule ya Msingi aliyosoma

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI MBEKENYERA MWAKA WA MASOMO 2021**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri katika mihani wako wa darasa la saba mwaka 2020. Ninayofuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika shule ya sekondari **MBEKENYERA** mwaka 2021.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini na kuzifanyia kazi.

- (i) Fomu ya kupimwa afya ya Mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambulika na Serikali.
- (ii) Fomu ya mahitaji muhimu ya shule
- (iii) Fomu za sheria za shule
- (iv) Fomu ya habari za Mwanafunzi na Mzazi
- (v) Mkataba wa kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule pamoja na kutekeleza maelekezo mengine yatakayotolewa katika vikao hahali vya wazazi shuleni

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** hivyo kamilisha maandalizi mapema ili kuwahi kuripoti shuleni.

NB: Unatakiwa kuja na **Cheti cha kuzaliwa na picha (passport size)**

Nakutakia maandalizi mema

**KARIBU SANA.
“JUHUDI HULETA MAFANIKIO”**

.....
**HUSSEIN J. OMARY
MKUU WA SHULE
0783500203/0686618393**

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

Sare za Shule.

- a) Suruali mbili (2) za kaki (kwa wavulana) zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo (ziwe na turn up na marinda mawili kila upande).
- b) Sketi mbili (2) za kijani (kwa wasichana) za marinda ya kawaida zitakazoshonwa kwa unadhifu. Fundi atapatikana shuleni.
- c) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni.
- d) Viatu vya ngozi jozi (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda
- e) Soksi imara nyeupe jozi mbili (2)
- f) Nguo za michezo, bukta moja, T-shirt ya njano isiyo na maandishi na viatu vya michezo.
- g) Aje na sweta moja (1) rangi ya kijani liwe la kufuma.
- h) T-shirt moja (1) ya kijivu yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni

Mahitaji kwa ajili ya Taaluma.

- a. Counter book 12 siyo daftari ndogo(angalau quire 2)
- b. Kalamu za wino (blue/nyeusi) za kutosha, kalamu ya risasi pencil (HB) na rula ndefu 1 mkebe (oxford) 1
- c. Faili kubwa kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za shule
- d. Kamusi ya kiingereza (dictionary)
- e. Rim moja kila muhula

NB:

- *Shule itatoa chakula cha mchana kwa kuzingatia makubaliano katika vikao vya wazazi*
- *Gharama za matibabu na afya ya mwanafunzi zitashughulikiwa na mzazi mwenyewe Hata hivyo unatakiwa kulipia Tsh 5,000/= kwa ajili ya bima ya CHF iliyoboreshwa ili mtoto apate matibabu katika hospitali, vituo vya afya na zahanati bure.*

Vifaa vya Usafi

Mwanafunzi anaporipoti shule aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi:

- (a) Fyekeo (b) Fagio laini (c) Squeezer /dryer (1) (d) dawa ya chooni lita moja
(e) Jembe lenye mpini (f) Panga

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT’S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MBEKENYERA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 9,

RUANGWA.

DATE.....

REF. No.....

THE MEDICAL OFFICER.

.....
.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Mr/Miss.....

Please Examine the above named student and give us a regarding his/her suitability for Secondary School studies.

Student’s full name

- 1. Blood.....
- 2. Stool.....
- 3. T.B test.....
- 4. Syphilis test.....
- 5. Urine examination
- 6. Eye test.....
- 7. Chest.....
- 8. Ear.....
- 9. Spleen.....
- 10. Abdomen test.....
- 11. Pregnant test (girls only).....

I certify that the above pupil is suitable /unsuitable for studies

If unsuitable please give reasons.....
.....
.....

Name of MEDICAL Officer.....

Signature of Medical Officer.....

Date.....

Official Stamp.....

SHULE YA SEKONDARI MBEKENYERA
FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI NA
HABARI ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.

SEHEMU A: HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani).....
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Kabila
4. Mahali na Wilaya alipozaliwa
5. Shule alipomaliza Darasa la Saba
6. Kidato anachokuja kuingia
7. Michezo anayopendelea

NO	JINA LA MCHEZO
I	
II	
III	
IV	
V	
VI	

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja, Kiongozi wa Kwaya, Ngoma
Michezo n.k

	UONGOZI	SHULE	MWAKA
i			
ii			
iii			
iii			

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

Tarehe saina.....

HABARI ZA MZAZI

SEHEMU B:

Jina kamili.....

Kazi.....

Nyumbani.....

Kata.....

Tarafa.....

(a) Anwani ya Mzazi/Mlezi

(b) Namba ya simu/.....

(e) Dini

Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo.....

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya kusoma.

MimiMzazi/Mlezi ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe saina.....

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha unatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- h) Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele
- i) Shule haimfungi Mwanafunzi kuamini katika imani yake ila kwa muda maalum na siku maalum
- j) Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa wakati wa muda wa masomo
- k) Hatakiwi kuja na nguo za nyumbani shuleni
- l) Ajapo kuripoti, aje na Mzazi. Bila kuja na Mzazi hatapokelewa
- m) Hairuhusiwi kuendesha ibada wakati wa masomo
- n) Hairuhusiwi mwanafunzi kubadili dini akiwa shuleni.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule.

- 1. Wizi**
- 2. Uasherati na Ushoga**
- 3. Ubakaji.**
- 4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi ,cocaine, mirungi, kubeli n.k.**
- 5. Kupigana au kupiga**
- 6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.**
- 7. Kudharau Bendera ya Taifa**
- 8. Kuoau au Kuolewa**
- 9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule**
- 10. Kusababisha mimba ndani au nje ya shule.**
- 11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.**
- 12. Kukataa adhabu kwa makusudi**
- 13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi**
- 14. Kuchafua kuta za shule**

**MKATABA WA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE
PAMOJA NA KUTEKELEZA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA
KATIKA VIKAO HALALI VYA WAZAZI SHULENI**

Mimimzazi/mlezi wa

kazi yangu ni.....mahali ninapoishi ni

anuani yangu ni namba ya simu.....

Nimesoma kwa makini maelekezo na maagizo yaliyopo kwenye fomu hii ya kujiunga na shule ya sekondari Mbekenyera. Kwa hiari yangu nakubali mwanangu ajiunge na shule hii.

Ninahidi:

- a. Kuwa nitamsisitiza kuheshimu na kufuata taratibu, kanuni zote za shule
- b. Kuwa nitashiriki katika vikao mbalimbali vya wazazi vitakavyoitishwa shuleni
- c. Kuwa kutekeleza bila ubishi yote yatakayo kubaliwa/kuafikiwa katika vikao vya wazazi shuleni
- d. Kuwa nitafuatilia maendeleo ya mwanangu shule na kuhakikisha anakuja shule kila siku za masomo
- e. Kuwa nitakamilisha mahitaji ya shule kwa mwanangu kwa wakati
- f. Kuwa nitatekeleza maelekezo yatakayotolewa na wiraza na idara ya elimu katika ngazi zote

Endapo nitavunja mkataba huu basi nichukuliwe hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi

Saini ya Mzazi/Mlezi

Saini ya Mwanafunzi.....

Saini ya Mkuu wa shule muhuri.....